**Mwanzo**

*mwandishi,* Tope Folarin

*mfasiri,* N.S. Koenings

Aliniambia kwamba ningemhudumia peponi.

Alinisindikiza hadi shule kila siku. Shule ilikuwa kiasi cha maili moja kutoka nyumbani, na nilipokwishatimiza umbali wa futi mia chache, pale jengo la fleti ya familia yetu lilipoanza kupotea katika upeo wa macho yangu, alikuwa akijitokeza kando nami.

Sikumbuki umbile lake lilivyokuwa. Badala yake, mara nyingi kumbukumbu hutuitia umbo la mtu lililochorwa kijuujuu tu, kwa mbali: bibi kizee wa kizungu, nywele zake kavukavu, rangi ya kijivu, zenye kutoa taswira ya umri wa alionao, kidogo ameinama, kicheko chake chenye msururu wa mianya na ming'aro ya fedha. Lakini hisia za mguso wake ninakumbuka vyema. Ulikuwa poa, ukifanana na karatasi, na uliniletea faraja ya kushangaza katika siku zile za msimu wa mapukutiko zilizokuwa joto sana. Tukifuatana, mara nyingi alinipapasa kichwani, na kimya kikali kilizuka kuvinyamazisha vishindo vya asubuhi vilivyosikika karibu nasi. Kwa namna fulani, nililpokuwa naye, nilijihisi ni mzima, kana kwamba ninalindwa. Hakuwahi kunisindikiza hadi shule hasa, lakini, daima, tukiagana, maneno yake yalikuwa hayohayo: "Kumbuka, ukiwa mtoto mzuri hapa duniani, peponi utanihudumia."

Nilikuwa na umri wa miaka mitano. Maneno yake yalipendeza kiajabu. Mazito, na yenye kuvutia. Sikumfahamu, hata jina lake sikulijua, lakini mwaliko wake wa kila asubuhi ulikuwa wa ukarimu usoweza kupuuzwa. Darasani, nilijiuliza, je, kuwa mtumishi peponi kungekuwaje? Nilijiona nikimbebea ndoo zilizojaa maji, nikitembea juu ya njia za dhahabu, nikimkanda miguu yake wakati sauti za malaika zikisikika kwa mbali wakiimba nyimbo za kumsifu Mungu. Nilikisia kwamba

ningekuwa na kibanda changu mwenyewe cha kipeponi. Na ningekuwa na muda wa kuyashughulikia mambo yangu ya kipeponi pia.

Vyinginevyo, Peponi ningefikaje?

Siku moja nilimhadithia baba yangu kuhusu nafasi niliyoahidiwa na yule bibi. Tulikuwa tukizungumzia peponi, pahala ambapo Baba alipenda sana kupawaza, na nilimjulisha kwamba mimi nilikwishawekewa nafasi huko. Nilisema, "Nimeshampata mtu wa kumhudumia."

"Unakusudia nini?" Tabasamu yake ilikuwa ya kuonyesha upendo. Mapenzi aliyokuwa nayo juu yangu niliuhisi. Nilirudia. "Baba, mimi ninaenda peponi."

"Na huko utafika vipi?"

Nilimweleza kuhusu yule bibi kizee, na kibanda changu cha kipeponi, na njia za dhahabu. Baba yangu alinikodolea macho kwa muda, simanzi na masikitiko yakionekana mara moja kwenye wajihi wa sura yake. Na hatimaye, hasira. Aliinama akinikodolea macho. "Sasa nisikize. Mtu pekee utakayemhudumia peponi ni Mwenyenzi Mungu. Hutomhudumia mtu mwengine yeyote."

2.

Baba yangu ameniambia mara nyingi kwamba alihamia jimbo la Utah kwa sababu hakutaka kuishi alikoishi mtu mwengine yeyote. Binamu zake na ndugu zake waliondoka Naijiria kuelekea Athens, London, Rome, New York City, na Houston. Baba yangu alitaka kuwa Mmarekani, lakini aliutamani upweke, kwa hivyo aliamua kusafiri kwenda sehemu pekee ya Marekani ambayo hakuwa na habari zozote juu yake.

Aliondoka Naijiria mwaka 1979, baada ya chuo kilichokuwa Utah (Chuo Kikuu cha Jimbo la Davis) kumpatia nafasi ya kusoma katika programu yao ya uhandisi. Biharusi wake, mama yangu, alifuatana naye. Walifikia nchi ambayo haikufanana kabisa na nchi walioitarajia. Baba, aliyekuwa

mshabiki mkubwa wa michezo ya televisheni kama *Gunsmoke* na *Bonanza*, alipogundua kwamba kofia za mtindo wa ki-cowboy zilikuwa zimeshapitwa na wakati, alivunjika moyo, na, kwa huzuni, kitu cha kwanza alichokinunua Marekani – kofia ya ki-cowboy*,* kubwa, rangi ya kahawia – aliiiweka mvunguni kwenye sanduku lake.

Mama alitua Marekani akitarajia amani na upendo. Wakati Mama alikuwa mwanafunzi wa sekondari Lagos, aliposikiliza sahani za santuri ambazo baba yake, mfanyabiashara, alikuwa akizileta kutoka Ughaibuni, alishikwa na mapenzi kwa muziki ya vikundi vya sanaa *The Beatles* na *Bob Dylan*. Ingawa alijichorea picha ya nchi ambako upendo hushinda yote, ambako watu weusi na watu weupe hatimaye waliweza kuziweka kando tafauti zao, bali Mama na Baba walifikia eneo ambalo hakukuwa na watu weusi wengine kwa masafa ya maili nyingi, eneo ambalo lilitawaliwa na dini ambayo walikuwa hawajawahi kuisikia.

Lakini hii ilikuwa Marekani. Na walipendana. Walihamia fleti ndogo mji wa Ogden, Utah, na kuanzisha familia. Mimi nilitangulia, 1981, na mdogo wangu alifuata 1983. Asubuhi na mchana, wakati Baba alipokuwa darasani, Mama alikwenda kujionea mji ulivyo, na usiku, wazazi wangu walikumbatiana kwa mahaba, ndoto zao wakizipa uhai: Watazaa watoto wengine zaidi. Baba ataanzisha biashara. Watakuwa matajiri. Watoto wao watawapeleka masomoni kwenye shule bora. Watakuwa na wajukuu wengi. Watajenga tafsiri yao ya mbuga za peponi, juu ya kipande cha jangwa, katika nchi ambayo yenyewe ilikuwa ndoto, nchi iliyoelekea kutosadikika hadi walipoteremka kwenye ndege, wakiyakinga macho yao yasipigwe na jua, na kujionea wenyewe mtanuko wa ardhi ambao, miaka mingi iliyopita, Baba aliuonyesha kwa kidole kwenye ramani kongwe, bila ya matamanio.

3.

Nikitizama nyuma, hasa nikizingatia kilichotokea baadaye, siku zangu zinazobaki zikionekana zimekolea kwa sifa mbaya, ninaweza kugundua kwamba kulingana na miaka yote ya utotoni mwangu, miaka yangu mitano ya kwanza ndiyo iliyokuwa ya utulivu na ya kawaida zaidi. Tulihama sana miaka ile, lakini sikumbuki kitu chochote ila furaha.

Kumbukumbu ninayoipenda zaidi katika kipindi hichi: kwa sababu nisizozijua, namfukuza mdogo wangu katika fleti yetu nikiwa nimeshika penseli ya nta, ya rangi nyekundu. Ninapomfikia, ninambana ukutani na kulipaka rangi nyekundu kila jino lake, yeye akipiga kelele. Mama yangu anapomwona, anatoa ukwenzi; kutokana na nta nyekundu inayong'aa menoni mwake, anadhani mtoto wake anatokwa na damu. Ninapomwambia kwamba damu ni ya bandia, anacheka, na sasa sote tunacheka, na namruhusu mdogo wangu kunipakia rangi kwenye meno yangu pia. Halafu tunayapaka pia meno ya Mama – yeye akipendelea rangi ya kijani cha ndimu.

Maisha yalitiririka kama maji, vizuri, hadi tulipohamia Bountiful. Tuliamua kukaa pale kwa sababu Baba alipata kazi katika gereji, mji jirani wa Layton, na Bountiful ilikuwa ni moja ya sehemu zile chache zenye makazi rahisi na karibu ya kutosha na alikofanya kazi. Baba hakuweza kupata kazi ya uhandisi kokote kule kaskazini ya jimbo la Utah, lakini umekaniki wa magari alikuwa akiujua kidogo, na aliona afanye kazi hiyo hadi ipatikane kazi bora.

Ugonjwa wa mama yangu ulianza kujitokeza pindi tu tulipoingia nyumba yetu ya vyumba viwili, nyumba ndogo sana katikati ya mji, yenye kuta za manjano meupe na zulia gumu zilizoikunakuna miguu yetu. Sauti ya mama, ambayo awali ilikuwa kimya na laini, ikabadilika kuwa kubwa na ya kutisha. Makumbatio yake, ambayo zamani yalikuwa machangamfu na yenye kutuliwaza, yakaanza kuwa yasiyo na hisia, baridi na magumu. Na Mama akawa mkali – kila alipokasirika, alimrushia Baba vijiko na uma kichwani. Baada ya muda mfupi tu, akimrushia visu.

Asubuhi moja, mdogo wangu nami tulikimbia hima hima hadi chumba cha wazazi wetu kwa sababu tulimsikia Baba analia. Sikufikiria hata siku moja kwamba Baba angeweza kulia. Tulimwona Mama akisimama kando naye, akimtawala, macho yake yanachemka kwa ghadhabu. Baba alikuwa karibu uchi. Nguo zake zimeraruka, zimetupwa kila pahala chumbani mle. Baba alitoka damu kwenye paja, na mchanganyiko wa jasho na machozi, ukimeremeta kama nyota, ulitanda usoni mwake. Mdogo wangu nami tulinyoosha mikoni yetu ili tumfikie lakini Mama alitulaani akituamrisha tuondoke: "TOKENI HAPA WASHENZI NIYE!"

Nilijawa na hofu. Nilimtazama Baba. Mdomo wake wa chini ulitetemeka. Meno yake mekundu. "Ndiyo, nendeni!" alisema. "Mnasubiri nini? Tokeni sasa!"

Tulitii amri. Chumbani kwetu tulikumbatiana. Baada ya muda mdogo tu, Baba alianza kupiga mayowe.

Katika siku zilizofuata, mimi na mdogo wangu tulishuhudia tukio hilo hilo mara nyingi, baba akiianama chini, akitapatapa, mamangu akisimama kijeuri kando naye. Kila mama alipojawa na jazba, babu aliipokea adhabu yake, na baadaye kuja kutuambia kwamba Mama hajisikii vizuri, lakini tusiwe na wasiwasi, Mama tunayemjua atarudi katika hali ya kawaida, tukiwa na matumaini kwamba atapona. Na sisi tulimwamini kwa sababu tulikuwa hatujautambua ukali na uzito wa ugonjwa wake.

Hatukuchukuwa muda kuugundua ukweli. Baada ya Baba kwenda kazini kila asubuhi, Mama alijifungia chumbani mwao. Hakujihusisha sana nasi, lakini mara kwa mara alifungua mlango na kutuomba tuingie. Alituomba kusimama pembeni, karibu na kabati. Alielekeza kidole sehemu mbalimbali: pale alipozihifadhi nguo zake, pale penye dawati la Baba, na sehemu tupu karibu na kioo chake kirefu. Akituuliza kama sisi tuliona pia.

"Tukiona nini, Mama?"

"Hamwoni? Mna matatizo gani?"

Mdogo wangu nami tulitazamana. Ulikuwa mchezo?

“Mama, sioni kitu. Ruhusa kutoka sasa?”

“Hapana. Hamwondoki hapa mpaka mkiniambia kwa nini kile kitu kipo hapa. Niambie kwa nini hakiondoki!”

Mara nyingine, mimi na mdogo wangu tulimdanganya. Tulimtungia hadithi kuhusu kile tulichokiona, na Mama aliashiria kwa kichwa kama vile kuna kitu amekifahamu. Mara nyingine alikataa, akituambia tutafute tena. Daima tulichanganyikiwa. Tulikuwa na wasiwasi. Ingeweza kuwa mchezo, na pengine tungeufurahia, lakini macho ya Mama yaliyokuwa kama ya mnyama wa porini, yalituhangaisha.

Alikiona kitu ambacho sisi kamwe hatukukiona, katika vurugo la akili zake gonjwa, kijikitu kidogo kilikua na kusitawi, kikimtesa.

Mara alituambia bora tuondoke kabla hawajaja kutukamata. “Kuna kitu pahali hapa kisicho sawa,” alisema. “Si sawa kabisa.”

Alivuta shuka kujifunika, aliwasha redio, halafu kujibembeleza hadi alale.

4.

Nilianzia shule tarehe saba, mwezi wa tisa, 1987, wiki chache tu kabla ya kutimia umri wa miaka sita. Nilifurahi, kwa sababu, mara nyingi kila asubuhi, nilikuwa nikikaa nikiwatazama watoto wa mtaa wetu chini ya dirisha la chumba changu, wakielekea shuleni, vitabu mikononi, mifuko migongoni kana kwamba walikuwa wakielekea dunia nyingine. Nilihisi, kwa mbali, kwamba, shuleni, ningekuwa zaidi ya kaka au mtoto, kwamba kila siku ningerudi nyumbani nikiwa na ujuzi ulokuwa wangu tu, wa mimi peke yangu.

Siku ile ya kwanza, familia yangu walinisindikiza hadi shule, na ninakumbuka kwamba mkuu wa shule alinipa mkono. Mimi, kwa haya kidogo, nilimpa mkono wangu pia, na tukipeana mikono alisema “Tumefurahi sana kwamba umekuja hapa!”

Machoni mwake mulikuwa mna shaka. Namna alivyonitizama. Kana kwamba nilikuwa kijitu cha kutisha, kijitu kisichojulikana. Ndivyo nilivyojua kwamba mimi nilikuwa tofauti. Kwenye pembea, wanafunzi wenzangu waliomba kugusa nywele zangu. Niliwaruhusu. Ndipo Simon aliisugua ngozi yangu na kumkimbilia msimamizi wa uwanja wa michezo huku akibubujika machozi. “Rangi haitoki!” alilia. “Kwa nini haitoki!?”

Siku chache baadaye, nilimwuliza Baba kwa nini nywele zangu zilikuwa za kipilipili namna hii, na kwa nini, nilipokoga, rangi ya kahawia ya ngozi yangu haikutoka. Alianza kunizungumzia umuhimu wa kuwa na fahari, na maana ya kujiheshimu, lakini kwa kweli sikumwelewa vizuri.

Wakati akizungumza, nilimkumbuka yule bibi kizee niliyemkuta njiani nilipokuwa nikienda shule.

Asubuhi ile, Baba alinikumbatia kizingitini na kuniambia kwamba itanibidi nitembee peke yangu hadi shule kwa sababu alikuwa na kazi, na Mama alikuwa hajisikii vizuri. Nilisema “Okay,” lakini niliogopa kwa sababu shule ilionekana ni mbali sana.

Njiani, nikitembea kwa woga, kwa kusita, alizuka ghafla, kana kwamba nilimwunda kwa kumwota katika ndoto.

Aliniambia anaitwa Bibi Hansen, na aliniuliza ninafanya nini. Nilimwambia kwamba ninaelekea shuleni. Alitabasamu. “Sijawahi kumwona mvulana mweusi katika mtaa huu” alisema. “Unatoka wapi?”

“Natoka hapa,” nilisema. Alicheka, halafu akaweka mkono wake juu ya bega langu.

Tulipotembea, alizungumza, na nilipenda kuisikia sauti yake, ilivyopanda na kushuka kidogo, kwani kwa namna fulani, nilihisi si ngeni kwangu. Aliniuliza maswali kuhusu Baba na Mama na mdogo wangu. Alisema kwamba tokea alipokuwa mdogo alikuwa na hamu ya kwenda Afrika, lakini hajapata nafasi.

Tulipokaribia kufika shule, alinitizama machoni na kunigusa kichwani.

"Nimependa kuzungumza na wewe. Wewe ni mtoto mzuri sana." Pole pole aliyafumba macho yake na kuyafumbua akitingisha kichwa. "Wewe endelea hivyo hivyo. Labda siku moja utapata kunihudumia peponi. Ukifanya hivyo, ninakuahidi kwamba utapata kila kitu ulichowahi kukitamani maishani mwako.

Furaha niliyokuwa nayo nilipogeuka na kukimbia shuleni, furaha tupu ile, ni furaha ambayo tangu siku ile nimekuwa ninaitafuta.

5.

Asubuhi ile, niliamka kwa kumhisi mama anazipapasa nywele zangu. Nilipofumbua macho, Mama alitabasamu. Alikuwa mzuri sana. Amevaa nguo anazozipenda zaidi: shati rangi ya zambarau liliofumwa vizuri sana, kitenge kirefu chenye mawimbi, na kilemba chake kikielea juu ya misuko yake mikubwa iliyopendeza. Aliniomba nimwamshe mdogo wangu, na baada ya kutukumbatia, alituomba tuvae.

"Tunakwenda wapi, Mama?" nilimwuliza nikivaa suruali.

"Tunakwenda pahala pazuri sana!" Alicheka. "Sasa fanya haraka tusichelewe."

Mimi na mdogo wangu tulienda mbio katika giza lenye kibaridi kikali. Tulikimbia sebuleni, na tulipofika, Mama alitutazama mara moja akitupima kimawazo.

"Chukueni mikoba yenu na nguo pia."

"Tunakwenda wapi!?"

"Nimekwishawaambia, tunakwenda pahala pazuri sana!"

"Na Baba, je?"

Mama aligeuka na kuutizama ukuta. "Atakuja baadaye, baada ya kazi."

"Na shule, je?" niliuliza. Kule chekechea nilikuwa nimetimiza mwezi mmoja tu.

Mama alinionyesha nusu tu ya kicheko. "Usiwe na wasiwasi. Wewe jiandae tu."

Tulirudi chumbani na kuijaza mikoba yetu na soksi, chupi, mashati na suruali. Baada ya dakika chacke, tulirudi sebuleni.

"Tuko tayari!" tulisema kwa pamoja.

Alicheka.

"Mlifanya haraka kweli, ninyi! OK, subirini sasa, kuna mtu anakuja kutuchukuwa."

Tulikaa. Tulijaribu kuipuliza hewa ile baridi kwa umbo la duara. Mama aliingia chumbani kwake, na alipotoka alikuwa akiivuta nyuma yake begi la kusafiria lenye viringi. Mkono wake wa kulia ulikuwa umeshika sahani za santuri mbili-tatu. Badala ya kilemba chake, alivaa kofia kubwa ya ki-cowboy, rangi ya kahawia. Nilikuwa sijawahi kumwona Mama akifurahi alivyofurahi wakati ule.

Baada ya dakika chache, alikuja mtu kubisha hodi, na Mama alishiria kwa kichwa kwamba aliridhika.

"Nendeni! Hii ni sehemu ya safari yetu nzuri!"

Mimi na mdogo wangu tulikimbizana mlangoni, lakini nilimwahi. Kulikuwa na mwanamke amesimama pale. Nywele zake zilikuwa fupi, nyekundu, na vidoa kwenye uso wake vilivyoshikanashikana kwa wingi nilijiuliza vipi moja kiliweza kuishi, hivyo, bila ya nafasi ya kupumua ama kusitawi.

"Habari yake? Ama wewe mtoto mzuri, enh? Uko tayari?"

Mama alijiunga nasi pale mlangoni.

"Ndiyo, tuko tayari. Twende kabla hatujachelewa. Tuna mengi ya kufanya leo."

Tulipanda gari la bibi yule. Aina yake sikumbuki, ninachokumbuka ni kwamba lilikuwa dogo, na kwamba mama alinitaka nikae mbele. Yule mwanamke mwenye vidoadoa usoni aliwasha gari na kuigurumisha injini, Mama akimkumbatia mdogo wangu. Bibi alinigeukia na kuniuliza kama nilihisi baridi. Nilimwashiria hapana. Lakini tulikaa pale gizani hadi nilipohisi joto kwenye uso wangu na viatu vyangu. Halafu akaweka gia na tuliondoka.

Tulipopita duka la chakula la mtaa, duka la Smith, ghafla nilijua kwamba safari tuliyokuwa nayo haikuwa ya kheri.

"Mama, huyu mwanamke anatupeleka wapi?"

"Nimeshakuambia! Sasa nyamaza utulie."

"Mama, sikuamini. Tunakwenda wapi? Baba yuko wapi?"

Mama hakunijibu. Huyu mwanamke alinigusa kichwani na baadaye aliwasha redio. Stevie Wonder alikuwa akiimba, lakini sijui wimbo ulikuwa ni upi.

6.

Kilichotokea baada ya kungundua kwamba safari yetu haikuwa ya kheri, sikumbuki. Kama CD iliyoharibika, akili zangu zinasita na kuruka mbele, hadi kwenye chumba kidogo chenye kuta zisizokuwa na picha yoyote, huko YMCA, mjini Ziwa Chumvi. Siku zinaanza na mwalimu ambaye ananimiminia sifa; kila siku ananiletea vitabu vya kusoma, na ananiambia kwamba mimi ni hodari kuliko watoto wote ambao amewahi kukutana nao maishani mwake. Vingi vya vitabu vyake vinahusu viongozi Wamarekani Weusi, lakini mimi sijui bado Mmarekani Mweusi ni nani. Kwangu, wote wanaonekana ni weusi tu. Tunasoma habari za George Washington Carver, Booker T. Washington,

na W.E.B. Dubois. Pia ananihadithia maisha ya Martin Luther King. Nnapata kujua kwamba alianza kusoma katika chuo kikuu alipokuwa na umri wa miaka kumi na tano, kwamba alisomea chuo cha watu weusi kinachoitwa Morehouse, mjini Atlanta, na kwamba alipokuwa na miaka ishirini na sita tu, tayari amepata shahada ya tatu. Mengi mengine siyasikii, kwa sababu bado nnakifikiria chuo cha watu weusi kilichoko Atlanta. Atlanta uko wapi? Na kitu kama hicho kweli kinawezekana hapa Marekani? Watu weusi tu, watu kama mimi tu, katika chuo? Inaelekea haiwezekani, lakini hapo nnaamua kwamba lazima chuo, na mji wenyewe pia, ni mabaki ya enzi za zamani, hakuna tena. Mwalimu anacheka. Nywele zake nyeusi zinang'ara. Mikononi mwake, kitabu kinaonekana kipya kabisa, kana kwamba hakijafunguliwa na mtu mwengine yeyote. Anaugeuza ukurasa. Kilicho cha ukweli na kilicho cha uwongo mimi sijui tena.

Baada ya kusoma tuisheni, ninajiunga na mdogo wangu ambaye yuko nasari. Tunacheza pamoja mpaka afike Joy kutuchukua. Nywele zake ni ndefu, rangi ya dhahabu, na wajihi wake una mikunjo, umepauka. Anapendeza sana.

Anatupeleka sebuleni, na mdogo wangu anakwenda kukaa juu ya mapaja yake. Mchana hadi jioni, tunaangalia michezo ya televisheni, kama *Mahakama ya Wananchi* na *Hakimu*. Joy ananisugua kichwa kila mara, na, wakati wa matangazo, anainama kulibusu paji la uso wangu. Nadhani anafanya hivyo kwa sababu anajua ninavyomkosa baba yangu. Sijamwona tangu siku ile Mama alipotutorosha. Lazima anajua ninavyohisi upweke nikikaa mbali na baba, na kwamba niko tayari kufanya jambo lolote lile ili kuisikia tena sauti yake.

Mara kwa mara, marafiki za Joy wanajiunga nasi. Ninawakumbuka kwa mbali tu. Mmoja mnene, mmoja mwembamba. Kama mapacha wa kiajabu, wanarukaruka sebuleni, na kuzunguka kumbukumbu zangu pamoja na familia yetu ndogo ya kuazimia. Joy anapotupeleka chumbani kwetu,

mdogo wangu amelala, na mimi nimechoka kiasi kwamba Mama simwogopi.  Tunapofika mlangoni, ndipo hofu inarudi.

7.

Mara nyingine, Mama hajambo kidogo. Nnajua kwamba anameza madawa yake, na ingawa daima hana furaha, lakini angalau anajitambua.

Kuna siku ambayo hainitoki kabisa katika kumbukumbu zangu: mimi na mdogo wangu ilikua tunaingia shelta tukimtafuta Mama. Macho yangu yanalikagua jiko letu, upande wa kushoto, ambalo linameremeta kwa usafi, na chumba cha kupokea wageni, upande wa kulia. Katikati kuna meza iliyojaa vumbi. Mama anatoka chumbani. Amekuwa mdogo, amekonda. Macho yake makubwa, pua yake dogo kama kifungo. Anawasha redio, na kupata stesheni ya nyimbo zilizopendwa, na anaanza kuvuma. Mara tunawasikia *Mamas and Papas,* mara *The Rolling Stones,* mara *The Beach Boys*, mara *Simon and Garfunkel,* mara Bob Dylan, lakini, daima, lazima *The Beatles* watasikika. Akimsikia Paul anaimba, Mama anacheka. Siku zile, sikushangaa hata kidogo kumwona bibi wa Kinaijiria kuwa na mapenzi makubwa kama hayo kwa ajili ya *The Beatles.* Kitu cha pekee nnachokijali ni kwamba *The Beatles* wanamfurahisha. Mara nyingi nnatamani sauti zile zisizo na miili zingetuwaletea *The Beatles* tu, *The Beatles* juu ya wote, *The Beatles,* usiku kucha, ili Mama apate nafuu.

Tunapofika shelta, Mama anaacha kupika vyakula vya Kinaijiria. Atatengeneza vyakula vilivyoganda barafu tu, lakini mimi na mdogo wangu hatujali. Tunafurahi kila tunapomwona akijishughulisha katika jiko letu dogo, akifungua boksi la nyama ya kuku iliyoganda; tunaposikia kishindo kile kitamu cha foili inapochanika, mama akiweka foili pamoja na kuku kwenye oveni. Baada ya muda mfupi, moshi wenye harufu nzuri unatembea katika mianzi ya pua zetu. Katika sahani zetu, anatutilia saladi ya kaa ailyoinunua dukani, au, mara kwa mara, kama pesa zinamtosha, wali wa kukaanga kutoka kwa hoteli ya Kichina ya mtaa wetu, pamoja na yule kuku wa kukaanga.

Kabla hatujaanza kula, Mama anaizima redio, na kama ni wakati wa kiangazi, dirisha liko wazi, upepo vuguvugu ukichezea migongoni mwetu.

Kwa mujibu wa Mama, ukimya ni upendo.

Kwa hivyo, na sisi, kwa zamu, tunajifunza kuupenda ukimya. Tunapoingia, mama akikataa kututazama, anatuashiria upendo wake wa dhati juu yetu. Kama tukimwuliza swali akidharau, anatujulisha kwamba tuna akili za kutosha kuyashughulikia mambo yetu wenyewe. Tunapomwita, akikataa kuitikia, tunajua kwamba kwa vyovyote vile, anatukumbatia.

Anavyojua Mama, kumtambua mtu ni kumkasirikia.

Kama tukiyahisi macho yake juu yetu tunapofanya kitu, tunajua bora tuache kabla hajaingia jazba. Lakini mara kwa mara tunachelewa. Sauti yake inalipuka kutoka kwa koo yake, kwa mawimbi moto yanayoacha mapovu ya mate kwenye ncha za mdomo wake. Sauti yake inapanda hadi darini, na kuning'ing'ia huko, ikielea juu ya yote, panda la uso wake likitoka jasho, wakati sisi tunatizama mbele yake, tukijaribu kumwonyesha upendo wetu, kwa ukimya wetu. Mara nyingine, upendo wetu anaupata, anaupokea, na hasira zake zinaondoka juu yetu; jasho lake linakauka, na hatimaye anatabasamu, na vitu vyote hutulia.

Lakini, mara nyingi, hafahamu. Ukimya wetu unamwudhi nafsi yake. Anasahau alivyotufundisha tangu zamani kuhusu maana ya ukimya, na anatupigia kelele mpaka anachoka. Halafu anaketi chini, akiegemea ukuta, huku akilia kwa machozi hadi usingizi kumshika. Mdogo wangu nami tunaleta mablanketi kutoka kwa upande wetu wa chumba, na tunamfunikia mwili, halafu sisi tunajitafutia nafasi ubavuni mwake kuonesha mapenzi yetu kwake. Hiyo pia ni upendo.

8.

Kwenye shelta, daima niliota ndoto. Kuota ndoto wakati wowote kulikuwa sawa kwangu, macho yangu yakiwa wazi ama yakiwa yamefumbwa. Ilikuwa nikijiamsha makusudi, katikati ya ndoto, niliweza kuiendeleza ndoto hiyo mpaka usiku. Kwa hivyo nilijaribu kuamka mapema iwezavyo, ili kuutunza mwunganisho baina ya mimi na upande ule wa pili.

Niliota wakati nikifikicha macho nikielekea bafu. Niliota niliposafisha meno, niliota nikikoga. Nikiwaamsha Mama na mdogo wangu, tukianzia siku yetu kwa pamoja, niliota.

Katika kioo, wakati wa kusafisha meno, nilimwona baba yangu. Alifanana nami: pua yake pana, panda la uso zuri, la fahari. Nilimwashiria kwa kichwa kwamba ninamwona, na akanijibu kwa kufanya vile vile. Badala ya kuketi chini tukila, niliona kwamba bali tumekaa juu ya kochi zuri, mpya kabisa, sahani ya santuri aliyoipenda sana Baba ikicheza, nyimbo za Sonny Ade. Na ukimya wetu ukawa kicheko. Mama aliponibinya mgongoni, juu hadi chini, mikono yake yakawa laini na ya kuzizimua. Alinikumbatia wakati akiniadhibu. Makofi yake yakawa sawa na maji ya moto usoni mwangu. Machozi yangu yakawa matone ya maji yale yakitiririka kuanzia usoni mwangu mpaka sakafuni. Kila kofi lilinisafishia nia. Macho yake yalionekana yana hasira kwa sababu ya wekundu wake. Nilichukuwa raba yangu ya kindotoni na kuyafutia macho yake rangi nyekundu yote, mpaka yakawa tena meupe. Nipomaliza, hasira zake zilimalizika.

Niliruka, niliogelea, na katika mpira wa kikapu nilishinda. Hakuna mtu aliyewahi kuchukua muda wa kunionya kwamba ningelitofautisha niliyoyaona usiku na mchana, yawe mbalimbali, ningeliyafanya ya mchana yawe muhimu kuliko ya usiku. Yote yakachanganywa. Nilianza kuamini kwamba uchungu haukudumu, na kwamba nilikuwa hatua chache tu kutoka kwa kujifunza kuruka. Nilijua kwamba nitaota mbawa. Wakati wake haujafika tu.

9.

Mdogo wangu nami hatukumwona baba yetu kwa muda wa miezi mitatu. Baada ya kufika shelta, Mama alituambia kwamba Baba karibu atakuja kuishi nasi. Lakini baada ya wiki chache, alituambia kwamba Baba hataki kuishi tena nasi, kwa hivyo, labda tusingemwona tena. Hatukumwamini. Upendo wa Baba juu yetu, tuliujua kiundani, na hatukuamini kwamba Baba angeweza kutuacha hivyo.

Siku moja, hatimaye, yule bibi mzungu mwenye vidoadoa usoni alirudi na alituambia kwamba karibuni Baba tutaonana naye. Alituarifu kwamba tutaweza kumwona mwisho wa wiki tu, kutokana na uamuzi wa hakimu. Hakimu ni nani, tulijiuliza. "Msiwe na wasiwasi," alitujibu. "Mjueni tu kwamba mtakuwa salama. Tutawalinda."

Sikujua anazungumzia nini. Sikuwahi kuhisi kama siko salama nikiwa na Baba. Kutopata nafasi ya kunzugumza na hakimu kuliniumiza. Nilitaka kuingia televisheni kuzungumza na Jaji Wapner, katika mchezo wa *Hakimu*. Nilijua kwamba ningelikuwa naye kwa dakika chache tu, ningeweza kumshawishi kwamba sisi katika familia yetu tulihitaji kuwa pamoja.

Tulionana na Baba katika sebule ya shelta. Alilia machozi.

"Mnaendeleaje?" aliuuliza. "Hali yenu imekuwaje? Je, wamewaangalia vyema?"

Tulimlaumu.

Tulimwuliza, "Kwa nini hukuja kabla? Kwa nini ulituacha hapa? Wewe ulikuwa wapi?"

Baba alinyosha mikono kama mtu asiyejiweza, kama vile hana la kusema. "Sijui. Nipo hapa sasa."

Mdogo wangu alimkumbatia vizuri, na hata mimi sikuweza kujizuia, nilifanya hivyo hivyo. Baba aliishika mikono yetu, na niligeuka kumwona Mama yuko pembeni akitulaani kwa macho. Baba alimwambia kwamba ataturudisha Jumapili. Mama alitupa mgongo na kutoka.

Fleti yetu mjini Bountiful ilitupa hisia ya ugeni, ingawa bado ilikuwa vile vile tulivyoiacha. Baba alikuwa ameviacha vitu vyetu vile vile vilivyokuwa siku tulipochukuliwa kwenda shelta. Mwanzo tulikaa tu, tukitizamana. Hatimaye, Baba aliwasha televisheni na kutuomba kukaa mapajani mwake.

Jumamosi ile, *Hulk Hogan* alitutizama pale sebuleni akituonya vitamine vyetu tuvimeze, tuswali vizuri, na tuwaheshimu wazazi. Alikuwa mkubwa mno. Tulimwona akisokotana na adui mkubwa mwenye kutisha, na alikuwa anashinda, lakini adui mwengine aliingia ringi na kumpiga refa. Alimpiga *Hulk*. *Hulk* amebwagika chini, anaguna kwa maumivu, na yule adui wa kiajabu alitokomea mbali. Adui yule wa kwanza alimpiga *Hulk* kichwani, halafu akamzuia. Mimi, mdogo wangu, na Baba tulikaa kimya. *Hulk* akilala chini, akitoka damu, karibu atashindwa. Lakini alinyosha mkono juu, kuelekea mbinguni, na akaanza kuutingisha. Aliutingisha mkono hadi nguvu fulani kutoka mbinguni ilianza kutiririka ndani ya mkono wake, halafu kumwingia mwilini. Alitetemeka kama vile amejawa na nguvu mpya kabisa, na pole pole akaanza kuinuka. Akaendelea kutetemeka wakati adui yake akimpiga usoni na kifuani, halafu aliiunganisha mikono yake kufanya ngumi kubwa sana, na akaishusha kwa nguvu kwenye mgongo wa adui wake. Adui alizimia, na baada ya muda mdogo, refa, ambaye kachangamka tena, aliinua mkono wa *Hulk* kiushindi. Tulimshangilia tukikumbatiana. Usiku ule, baada ya Baba kutuweka vitandani na kututakia alamsiki, nilikaa macho kwa masaa mengi nikiunyosha mkono wangu kuelekea darini, nikiisubiri nguvu ya kiajabu iniingie mwilini.

Siku ya pili, tulikaa tukizungumza, lakini, jioni, Baba alituarifu kwamba ni lazima turudi shelta. Tulimsihi aturuhusu tuendelee kubakia hata kwa masaa machache, lakini alisema haiwezekani. Tukapanda gari tukiwa tumevaa vizuri kujikinga na baridi, na Baba akaturudisha shelta. Tulipoingia, tulimwona Mama, na akaja, akaishika mikono yetu, bila ya kumwambia Baba kitu chochote. Tulimsikia nyuma yetu.

"Theresa, unafanya nini?"

Kimya.

"Kwa nini unajaribu kuninyima watoto wangu nisiwaone? Kwa nini unavunja familia yetu?"

Mama hakusema kitu.

10.

Sikumbuki kuwa na mazungumzo mengi na mdogo wangu wakati huu. Bila shaka tulizungumza sana, lakini maneno tuliyoyasema siyakumbuki. Muda mwingi, nilikuwaninamuangalia kwa tahadhari. Mama alipotujia kwa hasira, nilimlinda, na katika nyakati ndefu zile za ukimya nilimnong'onezea. Nilifurahi kwamba Mama alitumia hasira zake juu yangu. Hata nilijihisi ni mkubwa, kila aliponibinya kandoni na mgongoni, kila akikusanya ngozi yangu baina ya kucha zake na kila mara kuiponza kwa nguvu zake zote.  Masusu yalikuwa moto na mekundu. Mara nyingine niliyahesabu, na kujiuliza ya mdogo wangu yalikuwa yepi.

Baada ya muda, lakini, niligundua kwamba Mama, kwa jumla, alisita kabisa kumjia mdogo wangu. Alinijia mimi kila mara, hata kama alikuwa anamgombeza yeye.

Baadaye akaacha kukasirika naye.

Aliponipiga, mara aliniita kwa jina la baba yangu. Sikujua la kumjibu, na nilipojaribu kumwambia kama mimi si baba yangu, alizidi kunipiga.

"Ujitambue," aliniambia baina ya makofi. Aliponibinya, alisema, "Usijaribu kuwa tofauti na vile ulivyo."

Sikuwahi kumwambia mtu kuhusu alivyonifanyia Mama. Niliamini kwamba ukimya wangu ulikuwa sehemu ya utu uzima. Kama ningemwambia mtu yeyote, ningekuwa ninaukubali utoto wangu. Sijui kama walimu wangu waling'amua yamhusuyo mama yangu, lakini kila siku zikienda,

ukarimu wao juu yangu ulizidi. Nilipigiwa mabusu na kukumbatiwa zaidi kuliko mtoto yeyote mwengine kule shelta.

Usiku mmoja, baada ya kunibinya mgongoni mote, Mama aliniuliza kama ninampenda. Nilimkumbatia kwa nguvu na kumwita mdogo wangu aje. Tulikaa pale chini tukikumbatiana kwa muda mrefu, ndipo Mama alituambia kwamba wakati wake wa kuondoka ulikuwa unakaribia kuwadia.

"Unakwenda wapi?" tulimwuliza.

"Nilivyo mgonjwa mimi, sifai kuwa kwenye dunia hii," alisema. "Sitokaa sana."

"Utanichukua?" alimwuliza mdogo wangu, akiwa na matumaini ya kukubaliwa.

Pole pole alitikisa kichwa chake. "Hapana. Ningependa, lakini hapana."

11.

Wiki moja kabla ya tukio, Mama aliingia sebuleni, akaniona nimekaa chini. Nilikuwa nimechoka sana. Nje, giza, na dirisha lilikuwa wazi. Upande mwingine wa chumba, mdogo wangu alikuwa amelala juu ya jamvi. Aliponijia, Mama alitabasamu. Mwangaza hafifu wa mwezi uliigusa sura yake.

Nilianza kutetemeka kwa kuhofia kwamba atanipiga tena. Alipoketi kando nami, nilipiga chafya kwa hofu. Alinyosha mkono, na niliinama, nikilisubiri pigo kali la mkono wake usoni mwangu. Badala yake, alinisugua shavu na nikaanza kulia.

"Una nini, wewe?" Mama aliuliza. Sikumjibu. Alishika mkono wangu. "Ninataka ujue, tu, kwamba sikuchukii," alininong'onong'eza. "Namchukia baba yako."

Sikusema neno.

"Ninamchukia kwa alivyonileta hapa, na ninamchukia kwa alivyonipa matamanio."

Niliashiria kwa kichwa kwamba nilikuwa nnamsikiliza.

“Wewe ulivyofanana naye, kumezidi,” alisema. “Na hii ndiyo sababu mimi na wewe kamwe hatuwezi kuwa marafiki.”

Niliinua uso na kumtizama.

“Itakuja siku utafahamu,” alisema. “Kila kitu nilichokifanya kitakuja kueleweka kwako. Utaona.”

Niliitikia kwa kichwa. Mama alinibusu shavuni, halafu akainuka na kuondoka.

12.

Mama alianza kumeza vidonge vyake mara nyingi zaidi, haikuchukuwa muda kabla ya kuwa anameza kila saa, na hatimaye kila baada ya dakika chache. Jioni moja, alipokuwa anatengeneza kuku wetu wa kukaanga, aliitupa chini boksi ya foili, akageuka, na akafungua kabati iliyokuwa karibu na friji. Alitoa kichupa kipya cha dawa, na kwa nguvu akatia kila kitu mdomoni, pamoja na vipande vya pamba. Nnakumbuka alivyozuiwa pumzi kwa pamba, akianguka chini kwa magoti na mikono kuvishika vile vidonge ambavyo alivitema. Alitambaa chini, mate yakimdondoka, akiviramba vidonge vyekundu na vya manjano kutoka sakafuni kama kiharara. Mdogo wangu nami tulimtizama hadi alipovimaliza. Alipokimeza kidonge cha mwisho, aliegemea ukuta na kucheka.

“Raha hiyo!” alisema.

Na akaanza kusinzia. Mdogo wangu akamkimbilia na alianza kumpapasa, halafu kumtikisa, ili asishikwe na usingizi. Jiko lilianza kutoa moshi, moshi mkubwa mwenye harufu ya sumu, na baada ya muda mfupi sote tulikohoa, ila Mama. Nilikimbia nje kumtafuta Joy.

Asubuhi siku ya pili, Baba alikuja kutuchukuwa. Tulipoingia fleti yetu, hakutuuliza maswali, bali alituambia tu tubadilishe nguo. Mdogo wangu nami tulianza kuogopa.

“Tunakwenda wapi?”

"Msiwe na wasiwasi. Harakisheni tu."

Nilianza kulia. Mdogo wangu alikimbia hadi kwenye chumba chetu. Bado tuliumiwa na kuathirika sana na tulichokishuhudia usiku uliopita, watu tusiowajua wakimshughulikia Mama, Joy akituondosha, akituambia kwamba Mama hajambo, ingawa tulimwona akikaa tu bila ya kuinuka, vipande vya pamba vikiwa vimetapakaa hapa na pale chini kando naye. Baba alimwita mdogo wangu arudi sebuleni. Alitabasamu.

"Njooni sasa. Mjiandae. Ninawaahidi kwamba mtafurahi."

Mdogo wangu nami tulivaa, tukamfuata hadi garini. Tulienda kwa dakika chache, mpaka tulifika mbele ya shule yangu ya zamani, shule nilikosomea kwa wiki chache tu kabla ya Mama kututorosha. Shule ambayo sijaiona kwa karibu mwaka mzima.

"Karibuni utarudi hapa," Baba alisema, akiionyesha kwa kidole. "Ujiandae. Ninawataka wote wawili muwe wanafunzi bora katika shule hii. Hamtokuwa na visababu."

Tukakaa tukilitizama jengo lile la matofali mekundu. Nilisoma ubao pale palipoegeshwa magari, karibu na mlingoti. Ulisema: Baraka za Siku ya Kushukuru! *Happy Thanksgiving!* Shule inaanzia tena tarehe ishirini na nane, mwezi wa Novemba.

Halafu, Baba akatupeleka kwenye maduka. Alitununulia keki za dalasini, na tulikaa kwenye viti vya chuma karibu na jengo la duka kubwa. Tuliwaona mama na baba wote wakikimbilia duka moja hadi jengine, wakiwa wamebeba mabegi makubwa mno mikononi mwao, wengine wakibeba watoto wao au wakiwavuta nyuma yao. Tuliona nyota ya bandia juu ya mti wa bandia, na theluji ya bandia iliyoenezwa juu ya zawadi za bandia pale chini ya mti. Nilijua bora nisimwulize Baba kuhusu zawadi zetu za Kirismasi. Tulitafuna keki zetu.

Wiki iliyofuata, Baba aliturudisha shelta. Alipotuona, Mama alitupa tabasamu dhaifu.

"Watoto wangu. Nimewakosa."

Alitukumbatia mmoja baada ya mwengine, na mimi alinishika kwa muda mrefu kuliko kawaida yake.

"Naomba radhi. Ninakupenda, mwanangu."

Tulienda chumbani pole pole, Mama akiishika mikono yetu.

"Nimewaandalia jambo zuri sana! Fumbeni macho."

Nilimhisi akitia kitu vuguvugu mikononi mwangu. Nilitizama chini na kuona sahani yenye vipande viwili vya kuku wa kukaanga, marahage kijani, wali wa Kichina, na, pembeni, biskuti yenye umbo la *Santa Claus.* Macho yake ya choklati na ndevu wa sukari, nyeupe kama pamba.

Kimya, tulikula.

13.

Mahakama ilikuwa kubwa sana kuliko nilivyotarajia. Sikufahamu walivyoionyesha yote ndani ya TV. Mimi na mdogo wangu tulipoingia, watu wote waliokuwemo walikaa kimya. Ilikuwa mara yangu ya kwanza, ninayoikumbuka, ya kuvaa suti.

Tulifikaje? Siwezi kukumbuka. Kurasa nyingi za kumbukumbu zangu zimepotea.

Hakim alikuwa mzee wa kizungu, lakini hakuwa *Judge Wapner,* tuliyemwona katika mchezo wa televisheni, wala hakuwa yule jaji kutoka kwa mchezo mwingine tuliokuwa tunautizama pamoja na Joy. Alipotuona alitabasamu.

"Msiogope wala msiwe na wasiwasi. Sote tupo hapa kwa kukitaka kile kitakachokuwa na kheri zaidi na ninyi," alisema.

Baada ya hapo, kuna kitu kilitokea, lakini sijui nini. Na pole pole jaji anakizungusha tena kichwa chake – kama pinduli kubwa yenye ndevu – atuelekee.

“Kazi yetu ya leo inaweza kuchukua muda mrefu,” anasema. “Lakini ninafikiri kwamba ninyi mnajua mtapenda kukaa na nani. Siwezi kuwaahidi kwamba lile mtakalosema mnalitaka ndilolitakalotokea, lakini maneno yenu nitayapima kwa makini sana.”

Mdogo wangu ananitizama, na nnahisi kama uso wangu unaungua.

Ninainama kutizama viatu vyangu, halafu ninamwangalia jaji, kichwa chake kikichezacheza kidogo tu, karibu mchezo wake usionekane, kutoka upande wa kushoto kwenda kulia, kama vile kilikuwa ni akrabu ya saa, ikihesabu wakati.

“Ninataka kuishi na babangu.”

“Una hakika?”

“Ndiyo, nina hakika.”

“Na wewe?”

Sote tunamtizama mdogo wangu, na kwa kichwa, anaashiria kwamba yeye pia, ndivyo anavyotaka.

14.

Je, baada ya siku ile mahakamani, Mama tulimwona? Sijui. Mara kwa mara, nikifumba macho na kusafiri kwa fikra nikiukumbuka wakati ule ulokua na dhiki na utata, ninamwona akinitikisia kichwa, akinikodolea macho kwa mtizamo uliojaa chuki, tukifunga mizigo chumbani kwake na kuondoka shelta kwa mara ya mwisho. Mara nyingi zaidi, lakini, hayupo. Hata kivuli chake hakiniamkii, hata upepo mkali baridi haupo. Katika msuko wa mambo, anatokomea. Anayayuka. Mdogo wangu nami tunarudi kwenye fleti ya Bountiful na tunaendelea na maisha yetu.

Ninaona aibu, na pia sioni aibu, kusema kwamba, siku za mwanzo, sikumkosa. Nilitaka tu kuruka mbali, masikitiko na huzuni kuwa nyuma yangu.

15.

Mama yangu anaishi Naijiria siku hizi, na sijui lolote kuhusu anayoyafanya na matarajio katika maisha yake. Yeye ni nani, anafanya nini, anavyotumaini kuwa. Sijamwona tangu alipoondoka. Sijui kama nitamwona tena.

Kuna maswali mengi sana ningependa kumwuliza.

Sasa, ninapomwaza yeye, ninamkumbuka yule bibi kizee aliyekuwa akinisindikiza shuleni kila siku. Ilikuwa kabla mama yetu hajatupeleka shelta, kabla hajapotea katika ukungu wa ugonjwa wake. Bibi Hansen aliishi katika nyumba mtaa mmoja na fleti yetu, na nilipoelekea shuleni, alikuwa anajitokeza kando nami. Alinidokeza machache kuhusu maisha yake, misukosuko aliyoyaona, maumivu aliokuwa nayo, halafu alinihadithia maisha yetu baada ya kifo yatakavyokuwa, na mazurimazuri yote yatakayomfikia baada ya kuiaga dunia. Nilipomwambia baba yangu kwamba nilitaka kumhudumia Bibi Hansen peponi, aliikamuakamua mikono yake na kuashiria kutofurahi kwa kutikisa kichwa. Aliniambia kwamba sitomhudumia mtu yeyote ila Mwenyenzi Mungu. Baadaye akamwita mama yangu na kumwomba anisindikize hadi shule siku ya pili. "Itakusaidia pia wewe kutoka kidogo," alimwambia.

Mama, mdogo wangu na mimi tulipokuwa tunaelekea shuleni, Bibi Hansen alizuka kando nasi, na alimwambia mama yangu kwamba yeye pia ataweza kumhudumia peponi. Bibi Hansen alikuwa ameshazeeka, na akili zake hazikuwa sawa, na miaka mingi baadaye nilipata kufahamu kwamba alikuwa mfuasi wa dhehebu la Mormon la zamani, ambalo katika kanuni zake, watu weusi, watoto wa kiume na wa kike wa Cain, hawawezi kuingia peponi ila kama watumishi.

Mama alisimama na kumgusa Bibi Hansen usoni. Alitabasamu. Alimwambia kwamba, tutakwenda peponi sote, sote tukiwa sawa, shida zetu zote za duniani tukiziacha nyuma yetu kwa milele, na jambo hilo si lilikuwa la kufurahisha mno? Bibi Hansen aliashiria kwa kichwa kwamba

ndiyo ingekuwa njema, halafu akacheka kama vile alijiwa na jambo zuri sana lenye kuridhisha. Alituacha akiyumbayumba, na sikumwona tena.

Ninamkumbuka Mama akicheka kwa ushindi tunapoendelea na safari yetu, uso wake umetulia, umependeza. Nilivyomwona siku ile kwa uzuri wake, alionekana mkamilifu.